**MAPITIO YA MWENENDO WA SOKO KWA WIKI**
**8 NOVEMBA 2024**

**KARIBUNI TENA KATIKA KIPINDI CHETU CHA KILA WIKI KINACHOKUHABARISHA KUHUSU MWENENDO WA SOKO LA HISA LA DAR-ES-SALAAM, NA KULETWA KWENU NA VERTEX INTERNATIONAL SECURITIES, PAMOJA NANYI LEO NI MIMI, FRANCO ATILYO**

Kwa wiki inayoishia tarehe 8 Novemba 2024, mauzo katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) yalishuka kwa kiasi cha asilimia 95.65, kutoka TZS 25.08 bilioni hadi TZS 1.09 bilioni na kiasi cha hisa zilizouzwa kilipungua kwa asilimia kubwa kutoka hisa milioni 21.10 hadi hisa milioni 1.60.

Jumla ya Mtaji wa Soko uliongezeka kwa asilimia 0.48, kutoka TZS 18.45 trilioni hadi trilioni 18.54. Mtaji wa Soko la Ndani ulipungua kwa asilimia 0.12, hadi TZS 12.29 trilioni kutoka TZS 12. 30 trilioni kutokana na kupungua kwa bei ya CRDB, DCB, MAENDELEO na NICOL.

CRDB ndiyo iliyoongoza kwa mauzo katika wiki hii ikirekodi TZS 926.88 milioni, ambayo ni 84.89% ya mauzo yote ikifuatiwa na DCB kwa mbali.

Kwa upande wa bei, TANGA ilipanda kwa TZS 40 wakati hisa za TWIGA zikiongezeka bei kwa TZS 60 huku za DCB zikishuka kwa TZS 5. CRDB ilishuka kwa TZS 10 NICOL ikishuka TZS 20.

Wiki hii ilishuhudia hisa za CRDB zikitawala kwa wingi huku katika mauzo kwenye kaunta ya kawaida ya biashara huku wawekezaji wa ndani wakiendelea kutawala mauzo ya soko wakirekodi jumla ya TZS 1.05 bilioni na hivyo kuendelea kuimarisha matarajio ya ushiriki mkubwa zaidi katika wiki zijazo.

Katika wiki kulikuwa na miamala 101 kwenye soko la hatifungani, ambapo soko lilisajili TZS 52.13 bilioni.

Mnada wa Hatifungani za muda mfupi namba 1164 uliofanywa tarehe 6 Novemba 2024, ulivutia zabuni 65 ambapo zabuni 58 zilifaulu. Jumla ya fedha zilizopatikana ni TZS 300.28 bilioni.

**MPAKA HAPO TUMEFIKIA MWISHO WA MAPITIO YA SOKO LA HISA LA DAR ES SALAAM KWA WIKI ILIYOISHIA IJUMAA YA NOVEMBA 1, 2024. MPAKA WAKATI MWINGINE MIMI NI FRANCO ATILYO**